Mzuka wa ruzuku

Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza.

Waandishi:
Richard Mabala na Churchill Shakim

Mchoraji:
Daniel Mzena

Wahariri:
Justice Rutenge na Evarist Kamwaga, Twaweza

Usanifu:
Churchill Shakim

©Tamasha/Twaweza - 2013

Barua:
TAMASHA
S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania

Simu: +255-714-661-544
Baruapepe: vtamasha@gmail.com
info@tamashavijana.org
Wavuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakili nakutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Ndugu wasomaji,

Watoto wetu wanaenda shule, lakini je, wanajifunza? Majaribio ya Uwezo yanayofanyika nchi nzima yanaonesha kuwa wanafunzi wengi sana hawajui kusoma na kuhesabu. Moja ya sababu zinazochangia kukua kwa tatizo hili ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia. Shule za msingi na sekondari za umma zinapaswa kupokea ruzuku yaani fedha ya kununua vifaa hivi. Ruzuku isipofika mashuleni, watoto watapata elimu ya aina gani?

Tukae tu tukiangalia watoto wetu wakienda shule bila kujifunza chochote, au tufanye kitu kutatua tatizo hili?

Fuatilia hadithi hii kujua unachoweza kufanya.

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha.

Wahusika

Bonge
Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo na mkereketwa wa maendeleo

Bibiye
Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Mwenyekiti
Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mtendaji
Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

Mwalimu Mkuu
Rafiki wa Bonge anayeamua kuchukua hatua ya kushirikiana na vijana na wanajamii ili kuboresha elimu shuleni

Bibi
Bibi yake Bibiye, anayewaunganisha wanawake ili kuchukua hatua za kuboresha hali ya elimu

Loh! Huyu mwalimu mkuu mpya kiboko kweli. Mpaka anatuarifu sisi wazazi.
Mmh! Magumashi hayo! Ona ruzuku inavyoshuka.
RUZUKU KWA MIAKA MITANO ILIYOPITA
Yaani serikali inaleta hela kidogo namna hiyo? Wanakula tu!

Na hii shule yetu imenichosha. Kusoma hawasomi. Kazi yao kudai pesa tu.
Naona hili tangazo lingine. Elimu bure kabisa.
Kwani kuna nini?

Haya, na matokeo ya yale majaribio ya kusoma na kuhesabu yaliyofanywa na Shirika la Uwezo, Tanzania tuko wa mwisho. Hata kwa Kiswahili, Wakenya wametushinda.
Mmh! Watoto hawajifunzi chochote. Hata watoto wa darasa la saba hawawezi kujibu maswali ya darasa la pili. Si aibu hiyo!

Umeona ee! Kuchanga twachanga lakini elimu bure kabisa.
Kweli! Shule ina faida gani?
Nakuambia. Hayo matokeo yametufungulia macho sana.

Bora mwanangu alime kuliko...
Hapana baba. Tukishirikiana tunaweza kubadili hali hii.
Karibu tunywe mwalimu.

Bora hizi pesa unipe kama mchango wa shule.
Hapa hupati. Hawa ni wachangiaji wa baa tu.
Ili ule michango baada ya ruzuku? We mjanja bwana!

Si kweli. Kwa nini usisubiri matokeo ya jopo?
Jopo gani?
Unaona. Hauji kwenye mikutano utajulia wapi? Ni jopo la kufuatilia ruzuku wilayani.

BAADA YA WIKI MOJA
Mwalimu mkuu amesema ukweli kabisa.
Na katika hizo kuna mgawanyo.
RUZUKU SH. 1000
Na kitabu kimoja si chini ya shilingi elfu tatu. Mwalimu atanunua wapi?

Kama serikali haitaki watoto wetu wasome, basi. Waache wasomeshe wa kwao tu.
Jamani mimi mtoto wenu si nilisoma hapa! Hebu tuchange kidogo. Mabadiliko ni sisi pia, tusisubiri serikali.
Tumechoka na michango. Kama serikali haitimizi wajibu wake basi na sisi hatuno. Tuondoke!

Sikiliza Bonge. Nilifurahi sana kurudi nyumbani. Lazima watoto wetu wapate elimu. Lakini ona hali hii.
Kweli kazi unayo Bwana. Si unaona wazazi wenyewe?

Lakini tuache mambo yalivyo? Lazima tubadilishe hali.
Na ruzuku? Ahadi kibao utoaji dafrao!
Hapo sasa. Serikali kama baba wa nyumbani! Lakini hakuna kulala...

Wanaume bwana. Kwa nini ni wapinga maendeleo namna hii?
Kulikoni mwanangu?
Wanatumia uhaba wa ruzuku kama kisingizio. Eti hawawezi kulipa.

Wewe si unajua mwanangu. Mbona baba yako hakushughulikii.
Najua mama. Lakini sasa tuna mwalimu mpya mzuri, mbona hatutaki kumwunga mkono?

Nimekusikia mjukuu wangu. Umesema vema. Ngoja sisi tuongee na akina mama wenzetu.
Kweli bibi. Asante sana
Akina mama twajua. Hata hii VICOBA mara nyingi ni kwa ajili ya watoto wetu kusoma.

Lakini si hivi tu. Akina mama tuchangie chakula cha shule maana tunaona watoto wanadhoofika kwelikweli.
Enhee. Na siku ile ya kukabidhi michango wawepo maafisa elimu tuwape ukweli wao.

Lakini we mwanangu, mkorofi sijawahi kuona. Hupai kabisa.
Nafaa sana. We anza na akina mama, mimi nitawahimiza vijana.

Tusipojitahidi, tutalaumiwa bure na watoto wetu.

Nyie wanawake sijui mnataka nini?
Badala ya kutafuta maendeleo, mnamwaga hela shuleni tu.
Shule ndiyo maendeleo baba.

Nawashukuru wote kwa kazi yenu kubwa. Michango yenu huleta uhai wa shule na uhai wa watoto wetu.
Makofi na vigelegele! Mheshimiwa Afisa Elimu umeona?

Sasa kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi, tutapata wimbo.
Shule yetu yafanana na gari.
Bila petroli haiendi mbali.
Michango yetu yaweza kuwa oili.
Petroli ruzuku ya serikali.

Nawapongeza sana kwa kazi hii nzuri. Ni mfano mzuri kwa watu wote. Na upande wetu serikali inajitahidi...
Kujitahidi si ahadi. Tumetoa na sisi ili na nyinyi mtekeleze ahadi zenu.

Mna maana gani?
Shule yetu inapata ruzuku kidogo sana. Tuambie kwanini inapungua kila mwaka.

Gari haliwezi kwenda kwa ahadi ya petroli tu.
Tunawagawia tunachokipata.
Tunashukuru. Lakini kama baba, serikali lazima iambiwe kwamba haitoshi.

Tunabishana nini? Tunapurahi kwamba tuna pesa za kuvalisha wanapunzi wetu. Hakuna kulala darasani tena. Sasa wapate pia vitabu. Kidole kimoja hakivunji chawa.
Nilinunua daftari lenye yale majaribio ya Uweco. Nitawapa nakala ili tuwe tunawapima watoto wetu sisi wenyewe.

MICHEZO
MZUKA WA RUZUKU

Je wajua?

Shule za msingi na za sekondari za umma zinapaswa kupokea ruzuku kila mwaka. Ruzuku hii inatolewa kulingana na idadi ya wanafunzi. Kwa mwaka:

- Shule za msingi zinapaswa kupata 10,000/- kwa kila mwanafunzi
- Shule za sekondari zinapaswa kupata 25,000/- kwa kila mwananfunzi

40% ya ruzuku hii inapaswa kutumika kununua vitabu vya kila somo. Pesa zinazobaki zinatumika kwa ajili ya zana za kufundishia, ukarabati mdogomdogo, utawala na gharama za mitihani.

Pesa hii si ya siri. Mwalimu mkuu wa kila shule ya umma anapaswa kubandika mapato na matumizi ya ruzuku kwenye ubao wa shule ili wanafunzi na wazazi wote waweze kusoma.

Katika hali ya sasa, shule nyingine bado hazipokei fedha ya ruzuku kwa mwaka, na hata hizo ambazo zinapokea zinapata kiasi kidogo sana kulinganisha na kile ambacho kimeahidiwa. Kwa wastani kwa miaka minne iliyopita, shule zimepokea kama 2000/- kwa kila mwanafunzi kila mwaka. Ndiyo maana maendeleo ya mashule ni haba.

Tufanyeje?

Tukizingatia umuhimu wa ruzuku katika maendeleo ya watoto wetu shuleni, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba shule zinapata ruzuku hii.

- Tufuatilie kama pesa za ruzuku zinafika shuleni kwetu.
- Tukague mbao za matangazo shuleni kuona kama taarifa ya ruzuku imewekwa hadharani.
- Tuwahoji walimu wetu na viongozi juu ya pesa hizi na tujadili pamoja ili tuamue tufanye nini.
- Tujitoe pia kwa hali na mali kuhakikisha kuwa watoto wetu wanapata elimu bora.
- Tukague madaftari ya watoto wetu, tusome pamoja nao na tuwapime sisi wenyewe kujua kama wanajifunza au la.

Kumbuka:
MABADILIKO NI SISI!

Je, umewahi kufanya jambo lolote la kishujaa kama Bonge na Bibie?

Au unamfahamu mtu mwingine aliyefanya kitu cha kipekee kuisaidia jamii yake?

Kama jibu ni ndiyo, tungependa utusimulie!

Tafadhali tutumie hiyo stori yako iliyoleta mabadiliko hapo unapoishi au iliyotokea mahali pengine.

Tunaweza kuitumia stori yako kuandaa vijitabu au vipindi vya Televisheni na redio ili kuelimisha wengine. Usikose kutumia fursa hii!

Anuani:
Barua: Twaweza-Shujaa, S.L.P 38342, Dar es Salaam
Barua-pepe: shujaa@twaweza.org
Simu: Tuma ujumbe mfupi (SMS) bure ukijumuisha neno SHUJAA kwenda **namba 15381**